## *Siku ya Kiesperanto 2026: Maendeleo Endelevu na Kujitolea*

Tarehe 26 Julai, tunaadhimisha Siku ya Kiesperanto, tukisherehekea kumbukumbu ya miaka 139 tangu kuanzishwa kwa lugha ya kimataifa ya Kiesperanto.

Kiesperanto kilizaliwa kutokana na lengo rahisi lakini muhimu sana : kuwaleta watu pamoja kupitia mawasiliano yenye usawa.

Zaidi ya kuwa lugha iliyoundwa kimakusudi, inawakilisha harakati za kimataifa zinazochochewa na kujitolea, ushirikiano, na heshima kati ya tamaduni mbalimbali.

Kujitolea ni nguzo muhimu ya mashirika ya Kiesperanto duniani kote, sambamba na kuheshimu Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu na, hivi sasa, kuchangia katika Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Kimataifa.

Kazi ya mashirika haya inakuza mitandao ya kimataifa ya mshikamano, ujumuishaji, na ushirikiano, huku ikisaidia kupunguza ukosefu wa usawa na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa.

Kwa mfano, ufundishaji wa Kiesperanto kwa hiari, unaolenga kupunguza vikwazo vya lugha na kupanua fursa za kujifunza, unachangia katika Lengo namba 4 kuhusu (Elimu Bora).

Vilevile, tunafanya kazi kufikia Lengo namba 16 (Amani, Haki na Taasisi Imara) kwa kukuza mazungumzo ya kitamaduni yanayozingatia usawa kati ya watu na kuwaunganisha watu bila utawala wa lugha moja, na hivyo kujenga utamaduni wa amani.

Kujenga dunia bora, yenye haki zaidi, na endelevu kwa wote kunategemea si tu sera za uma bali, pia utayari wa hiari wa raia wanaochagua kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote.

Kwa kuchanganya kujitolea, elimu, na mazungumzo ya kitamaduni, Kiesperanto kinaendelea kuonyesha kuwa jitihada hii ni ya pamoja.

Kama alivyo sisitiza Raisi wa sasa wa Baraza Kuu la Umoja wa Kimataifa Annalena Baerbock, sisi ni “bora zaidi tukiwa pamoja.”

Tunakaribisha jumuiya nzima ya kimataifa kuungana nasi katika kuchunguza matumizi ya Kiesperanto kama zana za kujenga ushirikiano unaozingatia usawa wa wote na kuthamini tofauti zetu.

Tutakutana Graz, Austria, kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti, kwa ajili ya Kongamano la 111 la Dunia la Kiesperanto.